Mpango wa Stampu za Chakula

10-1-2007

Mpango wa Msaada wa Chakula (unaojulikana pia kama Mpango wa Stampu za Chakula) ni mpango wa msaada wa lishe ambao hutoa kadi ya Vision (kadi ya matumizi ya plastiki) kwa watu wanaostahiki kwa matumizi ya kununua chakula kutoka kwa maduka ya mtaani ya vyakula. Hapa chini kuna muhtasari wa matoleo muhimu ya kustahiki Mpango wa Msaada wa Chakula. Habari kamili inayohusiana na kustahiki msaada wa chakula inaweza kupatikana kwa kuwasiliana na Ofisi yako ya mtaani ya Huduma za Jamii na Urudishaji 1-888-369-4777.

Watu Wanaostahiki

Mtu yeyote aliye peke yake, kaya, au kikundi cha watu wanaoishi na kula pamoja na ambao mapato yao na rasilimali ni ya chini na wanaofikia mahitaji fulani muhimu ya mpango wanaweze kustahili.

Mapato na Mikato ya Mapato

Mapato yote na rasilimali zote lazima ziripotiwe unapokuwa ukiomba. Ijapokuwa aina zingine za mapato zinaweza kutolewa, nyingi huhesabiwa katika kuamua ustahiki na kiwango cha manufaa ya msaada wa chakula cha kaya. Vizuizi vya mapato ya msaada wa chakula huenda juu kulingana na vile ukubwa wa kaya unavyoongezeka. Yafwatayo yanaweza kukatwa kutoka kwa mapato taslimu ya kijumla ya kila mwezi ili kuamua mapato halisi ya kila mwezi:

- kushughulikia gharama ya kaya, mkato wa kawaida utatolewa;
- kushughulikia gharama zinazohusiana na kazi na ushuru wa malipo, mkato wa asilimia 20 utatolewa kutoka kwa mapato yaliyopatwa;
- kushughulikia gharama ya ulezi wa anayetegemea mtu mwingine, mkato wa gharama asili, hadi kwa upeo unaoruhusiwa, utatolewa;
- kushughulikia gharama ya makao ya juu, mkato wa gharama asili, hadi kwa upeo unaoruhusiwa, utatolewa; na
- kushughulikia uwajibikaji wa kisheria wa malipo ya msaada kwa mtoto, mkato wa malipo halisi yatatolewa.

Kwa kuongezea, kaya ambazo zina washirika (wenye umri ewa miaka 60 au zaidi), au wale wanaopokea SSI, malipo ya walemavu ya Usalama wa Jamii, malipo mengine ya Wazee walemavu, au watu wengine walemavu wanaweza kukata:

- gharama ya matibabu ya zaidi ya $35 kwa mwezi iliyopatikana na mzee/mlemavu, ikiwa haijarudishwa au kukatiwa bima, na
- gharama zote za makao ya zaidi ya asilimia 50 ya mapato ya kaya yaliyorekebishwa.

Upeo wa Mapato Halisi ya kila Mwezi ni:

$851 kwa mtu 1
$1141 kwa watu 2
$1431 kwa watu 3
$1721 kwa watu 4
$2011 kwa watu 5
Ongeza $290 kwa kila mtu wa ziada

Rasilimali

Kaya zote zinaweza kuwa na rasilimali za hadi $2,000. Kaya zinaweza kuwa na $3,000 ikiwa mmoja wao ana umri wa mwaka 60 au zaidi au ni mlemavu.

Rasilimali zingine zimeruhusiwa, kama vile:

- Nyumba unayoishi
- Magari na motokaa zingine
- Hati za bima ya maisha
- Mali isiyohamishika inayoleta mapato (ikiwa rasilimali hiyo hutoa mapato kila mwaka na dhamana yake halali ya soko)
- Vifaa vya mwanabiashara na mashine za ukulima

Baadhi ya rasilimali zinazoweza kuhesabika ambazo zinatumika kuwadia upeo wa $2,000 (au $3,000) ni:

- Fedha, cheki na akaunti za akiba
- Dhamana za Akiba ya Marekani
- Vyeti vya akiba
- Mijengo au ardhi (isipokuwa nyumba ya familia)
- rasilimali zinazomilikiwa kwa pamoja

Matoleo Maalumu ya Wazee/Walemavu

Ikiwa kaya ina mtu mmoja ambaye:

1. ana umri wa miaka 60 au zaidi;
2. anapokea manufaa ya SSI au malipo ya ulemavu chini ya Sheria ya Usalama wa Jamii;
3. ni mzee mlemavu, mwenza mlemavu aliyeponea wa mzee, au mtoto mlemavu aliyeponea wa mzee; au
4. anafikia moja wapo ya vigezo maalum vya ulemavu,

inaweza kukata gharama ya kimatibabu ambayo haijarudishwa ambayo inapita $35 kila mwezi kwa mzee wa kaya au washirika walemavu. Mikato hufanywa kutoka kwa mapato ya kaya yaliyorekebishwa.

Kaya zilizo na watu wazee au walemavu pia zinaweza kukata gharama zote za makao ya zaidi ya asilimia 50 ya mapato ya kaya yaliyorekebishwa. Watu walemavu wanaopokea au kuomba manufaa ya SSI wanaweza kuomba msaada wa chakula kwa ofisi za mtaani za Usalama wa Jamii wakati wanapokuwa wakiomba au kuomba upya

manufaa ya SSI. Mchakato wa pamoja umezuiliwa kwa watu wanaoishi katika kaya ambazo washirika wote wanapokea au wanaomba SSI. Mtu mzee na mlemavu ambaye anaugumu wa kutembea anaweza kuuliza ofisi ya SRS ipange kumtembelea nyumbani au mahojiana ya simu. Mtu mzee na mlemavu pia anaweza kutaja mwakilishi aliyeidhinishwa, ambaye anaweza kukamilisha mchakato wa maombi ya msaada wa chakula kwa niamba yake au anaweza kumsaidia au kumzindikisha.

Matoleo Maalum ya Kaya zilizo na Mapato ya Shamba

Ikiwa gharama ya shamba inayoleta mapato inapita mapato inayopatikana kutoka kwa kujiajiri mwenyewe kama mkulima, hasara kama hizo sitaondolewa dhidi ya mapato yoyote yale yanayohesabu kwenye kaya. Ili kutumia toleo hili, mkulima ambaye amejiajiri lazima apokee au atarajie kupokea mapato taslimu ya kila mwaka ya $1,000 kutoka kwa kiwanda cha ukulima.

Matoleo Maalum ya Moja kwa moja za Kaya Zinazostahiki

Kaya ambazo washirika wote wanapokea au wanaidhini ya kupokea Msaada wa Muda wa Familia (TAF), Msaada wa Kijumla (GA) au Mapato ya Ziada ya Usalama (SSI) zinaweza kuzingatiwa kwamba zinastahiki moja kwa moja msaada wa chakula kwa sababu ya hali zao kama wapokeaji wa TAF, GA au SSI. Ikiwa washirika wote wa kaya wameidhinishwa kupata manufaa ya TAF, GA na SSI, wasiliana na ofisi ya mtaani ya SRS kuhusu uwezekano wa kustahiki moja kwa moja kupata stampu za chakula.

MPANGO WA STAMPU ZA CHAKULA UNAPATIKANA KWA WATU WOTE WANAOSTAHAKI, HAIJALISHI JAMII, RANGI, IMANI, JINSIA, UMRI, ASILI YA KITAIFA, IMANI ZA KISIASA, AU ULEMAVU.